# KANDA YA SHINYALU MTIHANI WA MWIGO
## KISWAHILI DARASA LA 7
## MUHULA WA TATU 2019

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.**

_1_ ni vitu kama vile madini, misitu,maziwa,wanyamapori na vitu vingine _2_ na maumbile ambavyo hupatikana katika mazingira. Mito pia huunda sehemu kubwa ya mazingira. Mto ni maji _3_ .  _4_ wakati wote,  _5_ kuanzia milimani kuelekea ziwani au baharini. Kuna baadhi ya mito _6_ hutowekea kwenye _7_ . Nchini kenya kuna baadhi ya mito na _8_ vingi. Mito mikuu ni pamoja na Tana, Ewaso nyiro na Athi, _9_ urefu wa kilomita 5477.  _10_ mingine ni Yala, Sondu, Malewa, Sio na _11_.
Mito maarufu duniani ni pamoja na amazon ulioko _12_ na mto nile unaoanzia _13_ hapa afrika. Bila shaka ni _14_ letu sisi _15_ kuitunza mito hii na mazingira kwa jumla.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. mazingira | B. maliasili | C. malighali | D. mazingara |
| 2. | A. vinavyotokana | B. zinazotokana | C. yanayotokana | D. wanaotokana |
| 3. | A. mingi | B. nyingi | C. makubwa | D. mengi |
| 4. | A. inayotiririka | B. yanatiririka | C. yanayotiririka | D. yanayotiririkwa |
| 5. | A. aghalabu | B. sanasana | C. mara mingi | D. kwa sababu |
| 6. | A. ambao | B. ambayo | C. ambazo | D. yenye |
| 7. | A. milima | B. mashimo | C. vinamasi | D. misitu |
| 8. | A. vishimo | B. vijitu | C. visima | D. vijito |
| 9. | A. wenye | B. yenye | C. zenye | D. Ambao ina |
| 10. | A. miji | B. mito | C. maziwa | D. misitu |
| 11. | A. mengineyo | B. nyingineyo | C. mingineyo | D. nyinginezo |
| 12. | A. ulaya | B. Asia | C. Uchina | D. marekani |
| 13. | A. Bara hindi | B. Bahari hindi | C. Ziwa viktoria | D. meditarani |
| 14. | A. wajibu | B. jukumu | C. tatizo | D. shughuli |
| 15. | A. wote | B. zote | C. sote | D. yote |

**Kutoka nambari 16-30 chagua jibu lililo sahihi zaidi**

16. Ni kihisishi kipi mwafaka katika sentensi
    ___! Tutaonana kesho
    A. Wallahi!    B. jamani
    C. inshallah    D. lo
17. Mzigo wake ni nanga ina maana
    A. hupatikana    B. ni mwepesi
    C. unaondoka    D. ni mzito
18. Kanusha: njooni na mle _______
    A. msije na msile
    B. msikuje na msikule
    C. njooni na msile

D. msije wala kula

19. Tambua maumbo haya
    A. kipenyo, moyo, kopa
    B. nusu duara, kopa, kishada
    C. duara dufu, kipenyo, moyo
    D. mche duara, kitovu, nyota
20. Chagua mpangilio bora wa maneno yaliyopigwa mstari katika sentensi. Gari <u>langu</u> liligongana <u>dafrao</u> na <u>lile</u> la jirani.
    A. Kiwakilishi, kimilikishi, kielezi
    B. Kielezi, kiashiria, kimilikishi
    C. Kimilikishi, kielezi, kiwakilishi
    D. Kimilikishi, kiashiria, kielezi
21. Kairo alijitosa majini chubwi! Akazama_____!
    A. Zaa
    B. Zii
    C. Jii
    D. gubigubi
22. Kitenzi lala katika kauli ya tendesha ni______
    A. lisha
    B. lalisha
    C. laza
    D. lalia
23. Fuko ni mnyama mdogo jamii ya panya aishiye shimoni, fuko pia ni
    A. mahali kuku hutagia
    B. kando ya barabara
    C. kitambaa cha kichwa
    D. sehemu ya nyuma ya meli
24. Juliet anaishi kusini mashariki ya rehema. Kwa hivyo rehema anaishi upande gani wa Juliet?
    A. Kaskazini magharibi
    B. Kaskazini mashariki
    C. Kusini magharibi
    D. magharibi
25. Ni lipi lisilo pambo la mguuni?
    A. Kishaufu
    B. Kikuku
    C. Njuga
    D. furungu
26. Ni sentenzi ipi iliyo na “ po“ ya wakati
    A watembeapo ni hatari
    B. Tulipofika tulilakiwa vyema
    C. Alipotorokea palijulikana
    D. Nilipomwona hapakunivutia
27. Tegua kitendawili?
    Mnazi wangu uko mlimani lakini nanywa madafu hapa.
    A. Moto
    B. Mlima
    C. Mvua
    D. mnazi
28. Mmea unaokua na kutupa mchele huitwa?
    A. mpungu B. mgomba
    C. mbuni D. mchele
29. Mshororo wa pili katika shairi huitwa?
    A. Tadhinia
    B. Uwili
    C. Mleo
    D. mloto
30. Neno SHINDA lina maana kahdaa ila;
    A. taabu B. kukaa kutwa
    C. faulu D. isiyojaa

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.**

Kiwanda cha umoja cha kutengeneza viatu vya aina ya ndara kilichoko mtwapa, kaskazini mwa mombasa,kimekuwa na maendeleo mazuri kwa sababu ya usimamizi mzuri, jitahada za wafanyikazi na ubora wa viatu vyake.

Ajabu ni kwamba kiwanda hiki kilifunguliwa miaka mitano tu iliyopita lakini kwa siku moja kinaweza kutengeneza viatu jozi elfu kumi na tatu na mia tatu. Pia inasemekana kwamba kwa mwezi kiwanda hicho kinaweza kutoa zaidi ya viatu laki tatu na elfu tisini na tisa. Ubora wa viatu vyenyewe umefanya viatu hivyo viuzike kwa urahisi hata nchi za ng'ambo kwani kizuri chajiuza chenyewe.

Marupurupu wanayopewa wafanyikazi, ni moja kati ya motisha zinazotumika kiwandani. Matibabu na elimu ya watoto wa wafanyakazi hao, pia hushughulikiwa vilivyo. Ndiposa wafanyikazi wasiopungua darzeni kumi na mbili wako tayari kufanya kazi usiku na mchana pindi wanapotakiwa kufanya hivyo, kwani wanajua kwamba „ushikwapo shikamana.

31. Viatu vya ndara ni viatu vya______
    A. kijeshi B. kanda mbili
    C. kutembelea D. wanawake
32. Sababu zinazofanya kiwanda cha umoja kufaulu ni_________
    A. 3 B. 4
    C. 5 D. 6
33. Kiwanda cha umoja______
    A. Kiko kusini mwa Mombasa
    B. Kina wafanyakazi mia tano
    C. Kina viatu aina nyingi
    D. Kinauza viatu hata ng'ambo
34. Kwa mwezi kiwanda kinatengeneza viatu vingapi?
    A. 399,000
    B. 39900
    C. 309900
    D. 3990000
35. Kamilisha methali : kizuri chajiuza_____
    A. Kwa bei nzuri
    B. Kwa bei ghali
    C. Na watu hukipigania
    D. Kibaya chajitembeza
36. Idadi ya wafanyikazi kiwandani ni _____
    A. 12
    B. 102
    C. 144
    D. 13300
37. Marupurupu ni malipo ya ziada. Je, malipo ya kujeruhi ni_________-
    A. Fidia
    B. Fichuo
    C. Kiokozi
    D. Mahari
38. Kwa nini wafanyikazi wa umoja wako tayari kufanya kazi usiku na mchana?
    A. Kule kutazamwa vizuri
    B. Kutaka pesa zaidi
    C. Kuogopa kushikwa wakigoma
    D. Kwa kuwa ni wengi
39. Viatu vya kiwanda hiki huuzika kwa wingi kwa sababu_______
    A. Wafanyikazi ni wengi
    B. Bei yake ni rahisi
    C. Viatu vyenyewe ni vizuri
    D. Vinauzwa huko ng'ambo

40. Maana ya methali “ushikwapo shikamana” ni
    A. Ukishikwa usibishane kubali
    B. Ukishikwa shindana usikubali
    C. Usikubali kushikwa ovyo ovyo
    D. Unaponufaishwa patunze

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50**

Kamaliza alizaliwa mwenye afya nzuri, mzito wa wastani, sura jamali, mwingi wa maungo na zihi ya umbo la mwili. Haiba yake ilizidi kukua. Shangazi yake, ambaye alikuwa mzee sana wakati huu, kama kawaida ya ajuza yeyote, hakusahau kumdekeza mpwa wake kwa tunu na tamasha.

Alipokua, alipelekwa shuleni kama ilivyokuwa ada ya nchi. Baadaye alipatwa na thari ya maradhi katika mwaka 1990, miaka mitatu kabla ya kijana huyu kutoka chuoni, ijapo alipata afueni baada ya siku chache, walakini sina yake haikurejea kuwa njema kama zamani. Mara aliporejea nyumbani baba yake alifariki dunia . kamaliza alipatwa na jitimai isiyo kifani. Lakini Bi. Komu alikuwa yungali makamo na alimpa mwanawe miangaza na kumliwaza ukiwa.

41. Kamaliza alizaliwa mwenye____
    A. Afya duni
    B. Uzani mwepesi
    C. Wajihi mzuri
    D. Mali kwa wingi
42. Kwa mujibu wa habari hii, kamaliza alilelewa _______
    A. Bila mapenzi
    B. Kwa masikitiko makubwa
    C. Kwa mapenzi
    D. Kwa jitimai isiyo kifani
43. Kati ya yafuatayo ni lipi ambalo kamaliza hakutendewa?
    A. Kupelekwa shuleni
    B. Kufarijiwa
    C. Kulishwa
    D. kulaaniwa
44. Baba ya kamaliza aliitwa?
    A. Shangazi
    B. Mpwe
    C. Bi.komu
    D. Bw. komu
45. Babaye kamaliza aliaga dunia mwaka gani?
    A. 1990
    B. 1993
    C. 1996
    D. 2000
46. Kamaliza alirejea nyumbani kutoka shuleni lini?
    A. 1993
    B. 1996
    C. 1990
    D. hatujaambiwa
47. Alipata afueni maana yake ni
    A. alipata nafuu
    B. alikuwa mahututi
    C. alipata tunu
    D. alipata dawa
48. Ajuza ni?
    A. Mwenye ujuzi
    B. Mwanamume mzee
    C. Mwanamke mzee
    D. Mzee sana
49. Jitimai ni sawa na______
    A. furaha B. tumaini
    C. vurumai D. majonzi
50. Kinyume cha ajuza ni_______
    A. sahibu B. shaibu
    C. saibu D. shahibu